

EBT ya Gonjwa-tandavu kwa Mwaka wa Masomo 2020-21 inakuja hivi karibuni!

EBT ya Gonjwa-tandavu au mafao ya P-EBT ni nini?

Kutokana na COVID-19, watoto wenye ustahiki wa milo ya shule ya bure au yenye punguzo la bei watapata mafao ya ziada ya chakula. Mafao haya ya chakula yanaitwa P-EBT. Mafao ya P-EBT yanazisaidia familia za Washington kununua chakula wakati shule zinapofungwa au zinapopunguza mahudhurio ya ana kwa ana.

Nani ana ustahiki?

Watoto wana ustahiki wa mafao ya P-EBT ikiwa:

- Shule yao imefungwa au imepunguza saa za mahudhurio ya ana kwa ana.
- Wana ustahiki wa milo ya shule ya bure au yenye punguzo la bei.

Familia zinatamaje maombi?

Habari njema: Familia hazihitajiki kutuma maombi ya Programu ya P-EBT! Ikiwa mtoto wako ana ustahiki wa milo ya shule ya bure au yenye punguzo la bei, anaweza kufuzu kiotomatiki. Familia zinapaswa kuhakikisha anwani yao ya sasa ya posta imehifadhiwa kwenye faili la shule ya mtoto na zinahimizwa kujaza fomu ya maombi ya mlo wa shule ikiwa kwa sasa mtoto wao hapewi milo ya bure au yenye punguzo la bei.

Familia zitapata kiasi gani?

Kiasi cha mafao kinatofautiana kulingana na muundo wa ujifunzaji wa shule ya mtoto kwa kila mwezi unaohusika. Kiasi cha mafao cha kila mwezi kitakuwa kuanzia \$25 hadi \$123.

Kadi ya P-EBT ina mwonekano gani?

Angalia barua zako kwa kadi yenye mwonekano kama huu! Kadi ya P-EBT ni ya kipekee na haichukui nafasi ya kadi ya chakula au ya EBT cash (Quest).



Kadi za P-EBT zitawasili lini?

Watoto wenye ustahiki wanatarajiwa kupokea notisi mwishoni mwa mwezi Machi, ambayo itakuwa na taarifa zaidi. Kadi ya P-EBT itatumwa peke yake kwa njia ya posta katika wiki zinazofuata.

Kadi za P-EBT zinatamaje?

Kadi za P-EBT zinaweza kutumika kama kadi ya benki kununua chakula kwenye maduka mbalimbali ya vyakula na masokoni, au kununua chakula mtandaoni kupitia Amazon au Walmart.

Familia zitapata kadi mpya ya P-EBT kila mwezi?

Hapana, familia zinapaswa kutunza kadi ya P-EBT ya kila mtoto. Utoaji wa kwanza utajumuisha mafao ya kuanzia mwaka wa masomo 2020-21 hadi Januari 2021. Mafao ya ziada yanaweza kuwekwa kwenye kadi kila baada ya miezi miwili hadi mwishoni mwa mwaka wa masomo kwa kadri dharura ya afya ya umma ya COVID-19 itakavyoendelea.

Tembelea dshs.wa.gov/PEBT ili kufahamu zaidi!

Ukhitaji taarifa hii kwa lugha nyingine, wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha EBT kupitia **833-518-0282**.

Familia zinahimizwa kushiriki katika milo ya shule ya **Grab-n-Go** hata kama wanapokea mafao ya P-EBT.

Taasisi hii ni mtoa fursa anayezingatia usawa kwa wote.



Washington State
Department of Social
& Health Services

Transforming lives